

SALA YANGU

Mgani V.C
17.07.2019 Arusha

mf

1. Bwa na, si ki a sa la ya ngu, na yo ma o mbi ya ngu,

f *p*

te na kwa ki nywa cha ngu, ni na ku si hi o na, mi mi dha i fu

mf

ka mwe, si we zi bi la we we, u li ye ngu vu za ngu, na te ge me o.

**Free
Organ
Fupi**

2. Uje, wakati wa usiku, nipate utulivu, nilalapo daima usiniache x2
Ona, shetani mwovu yeye, halali usingizi, haoni giza anatuwinda x2
3. Njoo, niamkapo mimi, nianze siku vema, iwe ni njema kwangu, yenye baraka x2
Tena, iwe ni siku nzuri, ya kupendeza kwangu, na familia yangu, na marafiki x2
4. Bwana, nilinde niendapo, na hata nirudipo, wewe nakuamini, niwe salama x2
Ona, maadui ni wengi, wanazurura ili, wanimalize ila, wanitetea x2
5. Nipe, baraka zako Baba, nifanikiwe leo, kwaajili ya mwili, na roho yangu x2
Tena, uwabariki ndugu, nao jamaa wote, wenye imani nawe, uliye juu x2
6. Wewe, ni kiongozi bora, uliye mwaminifu, mwenye ukamilifu, nakuamini x2
Osha, mapito yangu njia, iwe salama mwovu, awekapo mitego, aaibishwe x2